SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.20 NO. 2 2021
DOI: 10.51984/JOHS.V20I2.1767

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/index.php/johs

# Usawiri Wa Mwanamke Katika Utenzi Wa Vitimbi Vya Wanawake

Husin Hamed Husin Awhida

Idara Ya Lugha Na Taaluma Za Kiafrika, Kitivu Cha Sanaa, Chuo Kikuu Cha Sebha, Libya

**Keywords:**
Mwanamke
Jamii
Usawiri
Maadili
Maisha

**ABSTRACT**

Makala hii yenye madhumuni ya kueleza usawiri wa mwanamke kupitia utenzi wa Vitimbi vya wanawake. Ambapo mwanamke amechorwa ni mtu asiyeaminika, asiyejitambua, asiyejielewa wala kueleweka. Anayeongozwa na utashi wa nafsi yake na mbaya kuliko yote ni ile ya “samaki akioza mmoja kuambiwa wameoza wote”. Kwa kosa la mwanamke mmoja kuchukuliwa ni kosa la wanawake wote. Tatizo lililojitokeza ni kuona jinsi mwanamke alivyochorwa kuwa ni mtu anaejikomboa kutokana na mfumo mbaya wa ubabe dume katika jamii. Lakini mbinu au njia iliyotumika ni ya udhalilishaji kabisa. Kwani badala ya mwanamke huyo kuonekana amejikomboa kwa kutumia njia zinazokubalika kama vile; ya mazungumzo (siasa). Matokeo yake mwanamke huyo kuonekana amedhalilika zaidi. Katika kujipatia ukombozi wake. Mbinu zilizotumika katika makala hii ni ya maktabani. Kwa kuipitia matini husika na kuiona jinsi ilivyomsawiri mwanamke. Na mwanamke huyo kutambulika ni mtu wa namna gani katika jamii anayoishi. Makala hii imeeelezea historia ya mwandishi kwa ufupi, dhana ya usawiri. Nadharia iliyotumika katika makala hii ni nadharia ya mtazamo kike. Kwa lengo la kuonyesha jinsi gani mwanamke anahitaji kujikomboa dhidi ya ukandamizwaji wa mwanamme. Kwa umuhimu wa uchambuzi wa makala hii, imeeleza kuwa mwanamke ni mtu wa kuenziwa pamoja na kuthaminiwa na sio kudhalilishwa na kubandikiziwa kashfa juu ya kashfa ni hasara iliyoje. Kwani kila mwanaadamu awe mwanamke au mwanamme ana uhusiano wa namna moja au nyengine na mwanamke. Hivyo kumdhalilisha au kumgandamiza mwanamke ni sawa na mtu kujidhalilisha mwenyewe.

# صورة المرأة في ملحمة خدع النساء

حسين حامد اوحيد

قسم اللغات والدراسات الإفريقية، كلية الأداب، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
المراة
المجتمع
الصورة
الاخلاق
الحياة

**الملخص**

هذا المقال يسعى إلى توضيح صور المرأة فى الملحمة الشعرية : ( خِدَع النساء ) وفي هذه الملحمة، تصور المرأة على إنها إنسان غير مؤتمن، وغير ملتزم، وغير معروف للمجتمع.يصور مؤلفو الأعمال الأدبية المرأة بطرائق مختلفة في جميع الفروع الثلاثة الرئيسية للأدب المكتوب ؛ الرواية والدراما والشعر، ويسعى هذا المقال إلى إبراز صورة المرأة في شعر خداع المرأة.‘في هذه القصيدة ، يصور أفراد المجتمع المرأة على أنها : شخص غير موثوق به ، وغير مسؤول ، وواعي بذاته ، ويساء فهمه، ويعبر عنها بمفهوم سلبي في هذه القصيدة هو : "إذا تعفنت سمكة واحدة ، فكل الأسماك فاسدة"' يريد الشاعر أن يخبر المجتمع أن خطأ امرأة واحدة ، هو خطأ جميع النساء.‘ تستمر الحركات التي تقوم بها النساء في المجتمع لتحرير أنفسهن من النظام الأبوي في تشويه هذه الصورة في المجتمع، بدلاً من قبول التحرر الذي يناضل من أجله ، ليصبح أكثر إذلالًا.ويشير المؤلف إلى أن المرأة يجب أن تحظى بالحب والتقدير، وأن أي إنسان في العالم لابد أن يعامل المرأة بطريقة مختلفة.‘تتميز هذه القصيدة بأسلوب خيالي ، وفي هذه القصيدة يخبرنا الشاعر عن طريقة التحرير الوحيدة التي استخدمتها المرأة في المطالبة بحقوقها ، عندما كان

*Corresponding author:
E-mail addresses: Hus.awhida@sebhau.edu.ly
*Article History : Received 15 April 2021 - Received in revised form 11 October 2021 - Accepted 15 December 2021*

هناك عنف أمامها، فقررت المرأة في هذه القصيدة استخدام طريقة الخداع، ويوضح المؤلف أنه بهذه الطريقة يتحقق هدف التحرير/ولعل هذا هو سبب سماع المؤلف للنداء بداخله.

**1.0 Utangulizi**

Mwandishi ama mtunzi wa utenzi huu ambao ameutunga katika muundo wa tamthilia. Muandishi U. A. Fadhil amezaliwa mwaka 1945 huko Gede, Malindi, Mkoa wa

**2.0 Dhana ya usawiri**

Kwa mtazamo wa usawiri, inaonekana ni mkusanyiko wa hali au tabia mbali mbali zinazobuniwa na mwandishi wa kazi za fasihi, ambao usawiri huo hupewa muhusika katika hali ya ubunifu ambao hujitokeza katika matini ya kazi ya msanii. Hali inayomfanya muhusika aonekane ni mtu wa tabia gani.

Ameir (2011) anaeleza kuwa ni mbinu inayotumika kunasa hisia za wasomaji au pia wasikilizaji kutokana na picha za kimawazo wanazounda wasanii hao kupitia matumizi ya lugha.(2011:84)

**3.0 Nadharia ya mtazamo kike**

Ni nadharia ambayo kwa jitihada zake zote, imo katika kupambana na kujaribu kutatua matatizo yanayomkabili mwanamke. Katika zile jamii ambazo zinatawaliwa na wanaume. Inaaminika kuwa matatizo mengi yanayomkumba mwanamke, kimsingi yanatokana na jinsia yake. Mwanamke mbali na matatizo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii lakini bado anaonekana anakumbana na matatizo mengi akiwa kama mwanamke.

Nadharia hii ya mtazamo kike ilianza kupata mwamko mnamo karne ya kumi na tisa na kushika kasi miaka ya 60 na 70 na sasa ikiwa imeonekana kasi yake hiyo, kuongezeka mara dufu, katika kupigania ukombozi wa mwanamke. Ni dhana ambayo imejumlisha mikabala mingi ya kiuhakiki na mbali ya tofauti zao zinazojitokeza ndani yake, lakini bado inaonekana kukubaliana na kuwafikiana kwenye malengo ya kimsingi.

Njogu na Wafula (2013), wameelezea mtazamo huu kwa kupinga ile hali ya kukandamizwa na kuonewa mwanamke katika jamii kulingana na matwakwa ya kiutamaduni ambayo yanaendelezwa na jamii husika.

Ni nadharia ambayo imewekewa msingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa,na kiuchumi-pingu ambazo zimejengeka kwenye msimamo wa itikadi ya kiume. (2013:90)

Kutokana na mwelekeo huu wa mtazamo kike kulijitokeza matapo mbali mbali ya kimaeneo na kiitikadi. Kwa upande wa kiitikadi miongoni mwake, mulikuwa na ufeministi huru, ufeministi wa kiharakati, ufeministi wa kijamaa, ufeminiti wa kibidhaa, ufeministi wa kiutamaduni, ufeministi wa kiuyakinifu na ufeministi wa kidhanaishi. Haya yalielezwa na wataalamu akina Adamson, Briskin, McPhail. Walioelezewa na Njogu na Wafula (2013) pamoja na Wamitila (2002).

Kwa namna hiyo makala hii, imesimamia mhimili wa kuonesha kuwa ni nadharia inayokuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.

**4.0 Usawiri wa mwanamke**

Mwanamke kupitia katika utenzi huu wa Vitimbi vya wanawake amesawiriwa katika hali tofauti, zile zinazokubalika ndani ya jamii, na zile ambazo nyingi kati ya hizo zinaonekana ni zenye kumfedhehi mwanamke na kumtolea kashfa chungu nzima. Akiwa katumiliwa mwanamke Zainab (mke) kama ni mkombozi, kwa ushujaa aliouonesha wa kumkomoa Rashid (mume). Inaaminika kuwa katika jamii hakuna binaadamu mkamilifu. Udhaifu wa mwanamke ukachukuliwa kama ni bakora ya kumpiga nayo mwenyewe. Na huku ikisadikiwa ni njia moja wapo ya kumkomboa mwanamke huyo, kama mwandishi wa utenzi huu alivyoeleza.

**4.1 Usawiri wa mwanamke kupitia silka / tabia**

Mwandishi wa *Utenzi wa Vitimbi vya Wanawake* amemsawiri mwanamke ni mtu mwenye tabia njema. Kupitia masimulizi ya muhusika wake Salimu. Na tabia nzuri zinaonekana pale mwanamke anapojikubalisha kufata matakwa ya jamii yake. Kutokana na utamaduni wa jamii hiyo ulivyomfinyanga mwanamke na kumtaka awe hivyo alivyo.

**4.1.1 Mwanamke ni mtu msikivu, mtulivu na mwenye heshima**

Utamaduni wa jamii husika mara nyingi ndio unaoakisi hali ya mwanajamii kitabia. Ushahidi wa haya unapatikana katika ukurasa wa (10)

135 136
Salimu "Mbona ukinya huneni Salimu: Mkewe akamjibu
"Wafikiri jambo gani" "Sina yoyote ghadhabu"
"Na hali wako mwendani" "Wala linipalo tabu"
"Tusute hapa mekaa" "Nnangoja kuanziwa"

Mwandishi anaonesha jinsi mwanamke anavyokuwa na heshima na utulivu, hasa kwa mtu ambae hajamzowea bado. Haya yameelezwa na muhusika Salimu, kwa mtoto wake Rashid.Wakati maharusi wanarudi kwenye maskani mapya. Bi arusi alishindwa kuanzisha maongezi kwa mumewe kutokana na ugeni kwa mwenziwe. Mpaka Bwana arusi alipoamua kuanzisha maongezi hayo. Hapa inaonekana mwanamke anakuwa na heshima na utulivu kutokana na malezi na adabu alizokulia nazo katika jamii yake.

**4.1.2 Mwanamke ni mtunza nyumba: mpishi/ mle**

Ushahidi wa haya unapatikana ukurasa wa 5, 11 na 40 pale mwandishi alipomsawiri muhusika huyo, akiwa na sifa hizi.

69 70
Salimu: Kakulea wako mama Salimu: Tangu huwezi kusema
Kwa kite na kwa huruma Wala pia kusimama
Daima kikutizama Hata ndaa kikuuma
Huku kikupembejea Huwezi ila kulia

550 552
**Maelezo: Kutoka hapo mamake Maelezo: Kwa mikate ya sinia**
Muate ahangaike Kaimati na bajia
Ajili apate pike Na chapati nazo pia
Mwane kumuandalia Chai nono ya maziwa

582
Leila: Taposikia naosha
Vyombo vyangu nasafisha
Kusudi tajinamisha
Uwa tauegemea

Kutokana na maelezo ya beti hizo zinaeleza kuwa, mwanamke ndie mwenye kutunza nyumba yake. Kwa kuhakikisha familia yake inaendelea kuishi katika mazingira safi, usalama na siha kamili. Mwanamke ndie mwenye jukumu la ulezi kwa watoto wake. Mwanamke ndie mpishi katika nyumba yake. Haya yote hayaongozwi na jinsia ya kike, kutokana na maumbile yake. Bali yanatokana na uana ambao umempangia mwanamke kuwa ndie mwenye majukumu ya kazi za ndani.

**4.1.3 Mwanamke ni mwepesi wa kuomba radhi**Haya yamejitokeza katika ukurasa wa 16, 17, 21 kwa kumsawiri mwanamke na tabia nyepesi ya kuomba radhi.

224 226
Salimu: Linenda muangukia Salimu Kamuomba mavyaaee
Kwa mambo yalotokea Ende huko kwa mwanawe
Tena sitayarudia Rambi akamuombee
Majambo yaliyokuwa Yuwataka kuregewa
281 294
Salimu: Yale alipotamka Salimu: Mama hayalitamka
Mama nae lipomoka "Msamaha nakutaka"

Msamaha akitaka "Kwa yale yaliyotuka" Mwanawe kumwangukia "Kukuvundia muruwa"

295

Salimu: "ninajuta sikufite"
" Baba,nami usitete"
"Niteteza siniate"
"Hadi nihame dunia"

Mwandishi amemsawiri mwanamke kuwa, ni mtu anaekubali makosa yake. Pamoja na kuwa ni mwepesi wa kuomba radhi, ili kuweza kusamehewa makosa hayo. Mwandishi wa makala hii ameyabainisha hayo, kuwa hata mama anapomkosea mwanawe na akabaini kuwa ni kosa. Mwanamke huwa yupo tayari kuomba radhi ili kuondosha utesi baina yao. Na haya yanatokana na utamaduni wa jamii husika, kuonekana mwanamme ni shujaa. Kutokana na ushujaa huo, hawezi kuonesha udhaifu wa kutaka radhi pale anapokosea. Ila ni mwanamke ndie mwenye jukumu la kutaka msamaha huo.

**4:1:4 Mwanamke ni mwenye hadhi isiyokadirika**

Mwanamke ni mtu mwenye hadhi ya pekee, mwandishi ameyabainisha hayo katika ukurasa wa (6) alipomuelezea mama:

74

Salimu Mama wa mtu ni mama
Japo hana taadhima
Ni wako wewe daima
Hazuki wa kumkia

Mwandishi amemsawiri mwanamke kuwa ni mwenye daraja ya juu. Hadhi yake haina mithali. Hasa mwanamke huyo anapofikia hatua ya kuwa mama. Mwandishi anamweleza mama, hata awe ni mtu wa namna gani,bado hawezi kutokea mtu wa kuikiuka daraja yake. Haya yanaweza kulinganishwa na ile methali isemayo "*Mama ni mama ijapokuwa rikwama"*.

**4.2 Usawiri wa mwanamke kupitia silka /tabia mbaya**

Baada ya mtazamo wa mwanamke kuoneshwa kwa hadhi inayomstahikia kama mwanamke. Mwanamke pia amesawiriwa katika tabia mbaya. Tabia ambazo hazipendezi wala hazimpi mwanamke hadhi inayomstahikia. Na kuonekana mwanamke amejaa kashfa zisizokadirika. Mwandishi amemsawiri mwanamke huyo huyo katika tabia tofauti. Ili kukamilisha lengo lake. Kuwa mwanamke si mtu wa kuaminika, mwanamke ni kigeugeu. Pamoja na kukubaliana na msemo wa Kiswahili *"Hakuna kizuri kisicho ila"* Mwandishi amemsawiri mwanamke katika hali zifuatazo:

**4.2.1 Mwanamke ni muongo** Mwandishi amemsawiri mwanamke kuwa ni muongo. Ushahidi wa hayo unapatikana katika ukurasa wa 14, 20, 35, 52 na 54. Hali hii inajitokeza kupitia wahusika wake mbali mbali.

| 183 | 187 |
|---|---|
| Salimu: Mkwewe alimwambia | Salimu: Mame mwana kajipinda |
| Kwamba nana liumia | "sipitali kwanda nenda" |
| "Ukipoteza wakati" | "Kama kweli wampenda" |
| "Aweza kujifilia" | "Haraka ungekimbia" |

| 269 | 473 |
|---|---|
| Salimu: Kwa shogae amekwenda | Fatuma: Hilo ni jambo rahisi |
| Ajili kwenda kuranda | Kubwa ninayo nafasi |
| Hebu kaa hapo kwanda | "Nnakwenda kwa msusi" |
| Nnakwenda kuitia | Ndivyo nilivyomwambia |

| 474 | 475 |
|---|---|
| Fatuma: Sisi wake mabazazi | Fatuma: Au twende arusini |
| Wallahi hamtuwezi | Kule mbali Kibokoni |
| Mara twenda kwa shangaz | Kumbe tumo danguroni |
| Kumbe konani twangia | Riziki twajipatia |

| 500 | 501 |
|---|---|
| Sada: Safari za mazikoni | Sada: Au kukwamba ataka |
| Sizitilie saini | Ruhusa kwenda kusuka |
| Aidha na matangani | Heri ukampeleka |
| Asende yeye kuyaa | Simwate akajendea |

| 717 | 718 |
|---|---|
| Zainabu: Nisikiza mume wangu | Zainabu : Hakuna ila hasadi |
| Usijitie tewengu | Waja wanatufisidi |
| Hasadi za walimwengu | Hatufi ila ahadi |
| Tumeshadhihirishiwa | Itakapokutimia |

| 734 | 737 |
|---|---|
| **Zainabu:Maelezo:Huku matozi yatoka** | **Zainabu: Mamangu nnakwambia** |
| Mama nakupa hakika | Rashidi anaugua |
| Rashidi zimefyatuka | Heri kamba kumtia |
| Akilize, nahisia | Aula ataniuwa |

Mwandishi kupitia beti hizo, amemsawiri mwanamke ni muongo. Muongo wa kauli na mbinu za kupanga ili uongo wake utimie. Mwanamke huyo hana rika wala cheo. Akiwa yeye ni mama atakuwa muongo, akiwa ni mke atakuwa muongo. Maadamu yeye ni wa jinsia ya kike, nafasi yake katika jamii ni muongo. Ni hali inayotokana na mfumo wa ubabe dume, wenye kumuona mwanamke si mtu wa kuaminika.

**4.2.2 Mwanamke ni kuwadi**

Mwanamke amesawiriwa ni mtu mwenye tabia mbaya ya kukuwadia wake za watu. Ushahidi wa hayo umeonekana katika ukurasa wa 14, 20 na 32:

| 189 | 192 |
|---|---|
| Salimu:Sahiba litia shaka | Salimu: Mlango lipoushika |
| "Kwanini mama kushika" | Wali ndani mefungika |
| "Lazima yeye kutaka" | Na reza yalimeweka |
| "Nende bila ya rupia" | Kati kati sawa sawa |

| 193 | 194 |
|---|---|
| Salimu:Mkwewe kuona vile | Salimu: Sahiba lipotizama |
| Nyumbani asipakale | Wa mkewe yule mama |
| Alinyata pole pole | Nyumba alishaihama |
| Nde akakimbilia | Bila ya yeye kujuwa |

| 276 | 278 |
|---|---|
| Salimu: Sahiba kimtafiti | Salimu: Alipokisema haya |
| Akamwamba sikufiti | Mara mama litokea |
| Huyu ni wangu banati | Kwa vishindo kujitia |
| "Bibi kanitunukia" | Ndani, kuyashuhudia |

| 279 | 280 |
|---|---|
| Salimu: Pale pale kitandani | Salimu: "Waniasa raha zangu" |
| Rijali lilibaini | "Na huyu hawara yangu" |
| "Fujo hili ni la nini" | "Ilhali fedha zangu" |
| "Huyu bwana kumtia | "Wewe umezitukuwa |

| 433 | 438 |
|---|---|
| Sada: Mjukuu wangu sema | Sada: Hela usifanye pupa |
| Yalo ndani ya mtima | Moyo kakutapatapa |
| Maradhi yanokuuma | Nifikia kesho hapa |
| Nipate kukupa dawa | Saa nne kitimia |

Hapo mwandishi amemsawiri mwanamke katika tabia potofu ya ukuwadi. Ambapo anaonekana mwanamke kwenye daraja ya mama anamkuwadia mwanawe wa kike. Anamkuwadia mke wa mtoto wake wa kiume. Mwanamke daraja ya bibi anakuwadia wake za watu. Mwandishi amemsawiri mwanamke ni mtu mwenye tabia mbaya. Tabia ya kutokuwa mwaminifu kwa wake za watu.

**4.2.3 Mwanamke ni mchonganishi/fatani** Mwandishi ameendelea kumsawiri mwanamke katika tabia ya uchonganishi.Ushahidi wa uchonganishi huo ulivyojitokeza. Upo katika ukurasa wa 13 na 28. Kama beti zinavyojieleza:

176 383
Salimu; Bibi yule alinena Maelezo:Ilikuwa marufuku
Kumwambia wake mwana Mama yule kuja huku
"Mumeo nimemuona" Kwani ali ni mdaku
"Na mwanamke hawaa" Na fatani wa mtaa

Mwandishi amethubutu tabia hii mbaya pia kumpachika nayo mwanamke. Na mwanamke huyo akiwa ni mama. Kutokana na mfumo wa jamii unaoendeleza mfumo wa ubabe dume. Unaonekana ni mfumo wenye kumdhalilisha na kumgandamiza mwanamke kwa kumpachika kila jambo ovu.

**4.2.4 Mwanamke ni mzinifu**

Mwandishi wa utenzi huu amemsawiri mwanamke kuwa na tabia chafu ya uzinifu. Hali hii imejitokeza katika ukurasa wa 5, 6, 13, 14, 15, 43, 56 kama zinavyojieleza:

58 59
Salimu: Alikuwa na mkewe Salimu:Maishae siku zote
Yalimpate mpate Kwa wema kakaa nae
Ampatae yeyot Huyo mkewe mwishowe
Hachelewi kumtwaa Dereva kamtwaa

78 80
**Salimu: Mwenzangu wangu suhuba Salimu: Na mwengine mwanamke**
Alifikwa na msiba Heri yake nitamke
Ya mkewe kujiiba Kenda na shemegi yake
Na mwana alomzaa Na watu kuwasifia
178 179
Salimu: Ndipo mke akaanza Salimu: Kawa mke hachi tena
Tabiaye kugeuza Hishima aliikana
Na uovu kujifunza Vidume na vivulana
Uzinifu liuvaa Ikawa kwake hungia
196 205
Salimu: Huyu mkewe sahiba Salimu:Sahiba lisikitika
Ndani ali na jibaba Kwani alemdirika
Wali wenye wajiibaNi mtu alemwandika
Nyongo liwatumbukia Dereva wa motokaa

585 758
Leila: Utakapotegemea Maelezo: Akazitoa na kanga
Silahazo nje toa Zeinabu:Kiunoni hebu funga
Palipo na mwanya tia Takuonya unyakanga
Kazi itaendelea Kazi ninavyoijua
760 761
**Maelezo: Wakangia msowani Maelezo:Kwa kele akabaini**
Bibi na Bwana mgeni Rashidi: Mke wangu yuwazini!
Bwana juu, bibi tini Hebu jamaa ndooni
Rashidi aangalia! Muje kuyashuhudia

Mwanamke amesawiriwa kuwa amali yake ni zinaa. Iwapo mwanamke huyo ni mjane atazini ili apate mahitaji yake. Iwapo ana mume, iwe anatimiziwa ama hatimiziwi mahitaji hayo atazini ili kutosheleza utashi wake. Zaidi ya hayo amesawiriwa mwanamke ni mlipa kisasi kwa maovu. Kama hayo ya kufikia hatua ya kumzinia mume wake, mbele ya macho yake.

**4.2.5 Mwanamke ni mtenza nguvu**

Mwanamke amesawiriwa ni mtenza nguvu, kwa kulazimisha mambo yasiyomkinika. Ushahidi wa haya umejitokeza kwenye maandiko ya mwandishi, ukurasa wa 17,18 na 237 kama yanavyojieleza:

231 233
Salimu "Masikiziyo zibuwaSalimu: Mama haya litamka
"Usikize sawa sawa "Ambalo mimi nataka"
"Kisha nataka jibiwa" "Ni kuifuta talaka"
"Jawabu ilo na ndia" "Mwendo ulomwandikia"
236 237
Salimu: Mama alitakalamiSalimu: "Ninavyokwamba mie"
"Utwete wako ulimi" "Nataka umrudie"
"Hebu nisikize mimi" "Na yeye uishi nae"
" Ikiwa nimekuzaa" "Sahau yalotokea"

239 245
Salimu: Mama Kisema "Mwanangu"Salimu:"Usipolifanya hili"
"Ukitaka radhi yangu" "Basi nawe tuwe mbali"
"Ya Rasua na ya Mungu" "Tusijuliane Hali"
"Tenda ninavyokwambia""Hadi siku nafukiwa"

Mwandishi ameamsawiri mwanamke (mama) anavyoitumia vibaya nafasi yake. Mwanamke hatakiwi kumtenza nguvu mwanawe, kwa kufanya jambo lisiloyumkinika. Mwanamke ametumia silaha kali kabisa. Kufika hatua ya kumtamkia radhi mwanawe kwa jambo zito lisilowezekana. Baada ya mwanamke kumzinia mumewe na mume huyo kuamua kutoa talaka. Mwanamke (mama) anatakiwa zaidi kushauri na kunasihi badala ya kulazimisha.

**4.2.6 Mwanamke ni mwenye tamaa/hakinai**

Mwanamke amesawiriwa ni mtu mwenye tamaa na inda. Ni mtu asiyejuwa kukinai na kitu alichonacho. Ushahidi wa haya umejitokeza ukurasa wa 24,35,36 na 37 kama alivyoeleza mwandishi:

325 497
Salimu: Mke simuonye patoSada: Nnaanza kukufunda
Sababu ana kijito Wanawake wana inda
Kisha ni kama mtoto Nawe usipowatunda
Kukosa hakuzoea Kinyume watakwendea
498 498
Sada: Mwanamke atakalo Sada: Usimuoneshe kitu
Wewe kwako iwe silo Mfano chuma na kutu
Kila ataradhialo Takuwa hufurukutu
Siwe utamridhia Takavyokuhitajia
506
Sada: Usifanye kila mwezi
Kumkamatia mavazi
Siku kimwamba "siwezi"
Juwa atakununia

Mwandishi amemsawiri mwanamke ni mtu mwenye tamaa kupita kiasi. Pale mume akiwa nacho yeye ni muhitaji wa kupindukia. Na anapokuwa hana, basi huwa ni mwenye inda.Hivyo mwandishi anamtahadharisha mwanamme awe makini kutokumweleza mkewe uwezo wa mali alionao. Kumtunukia zawadi za mara kwa mara ili kuepukana na usumbufu na mashaka. Na hali hii ni kudhihirika kwa mfumo dume. Mfumo ambao unamkandamiza mwanamke na kumfanya dhalili.

**4.2.7 Mwanamke si mtu rafiki/ mwendani**

Mwandishi amemsawiri mwanamke kuwa si mtu wa kuwa mwandani na mumewe. Awe ni mtu baki kwake. Ushahidi wa hayo unapatikana katika ukurasa wa 24 alipoeleza:

326 327
Salimu: Na thuma na zako siri Salimu: Ovyo usiteke naye
Simuoneshe dhahiri Wala simdhihakiye
Kaa nae kwa hadhari Na lako usimwambie
Mno kumtunduia La kinyume na sharia
328
Salimu: Simpende akajuwa
Kwani atajizuzuwa
Na hishimae takuwa
Pungufu itapungua

Mwandishi amemsawiri mwanamke kuwa ni mtu asiefaa kupewa siri. Si mtu wa kumshauri. Mwanamme (mume) hafai kukaa akafurahi nae. Hata katika suala la mapenzi. Mwandishi amemshauri mwanamme asimpende mkewe mpaka akajua. Kwa kukhofia kutakakabari. Bado mwandishi anaendelea kumgandamiza mwanamke kwa haki yake. Na hii ni kutokana na mfumo dume uliotawala.

**4.2.8 Mwanamke msaliti wa ndoa**

Mwandishi amemueleza mwanamke kuwa ni msaliti, hana uaminifu katika ndoa yake. Ushahidi wa hayo umeonekana katika ukurasa wa 34 kwa kueleza:

471 585
Fatuma:Mume angawa na pesa Lela: Utakapotegemea
Bali sisi atuasa Silahazo nde toa
Ndipo tukipata fursa Palipo na mwanya tia
Tukawa twajizinia Kazi itaendelea

Mwandishi amemsawiri mwanamke ni msaliti wa ndoa yake. Hana subira katika ugumu anaopambana nao katika maisha ya ndoa. Mathalan mume akimzuilia matumizi ama kutompa ruhusa kutoka nje. Mwanamke huwa mwepesi kuuza utu wake, kwa kumuendea mumewe kinyume.

**4.2.9 Mwanamke si mwaminifu**

Mwandishi wa utenzi huu, amemsawiri mwanamke kuwa si mwaminifu. Ushahidi wa haya unaonekana katika ubeti wa 49 wenye maelezo yafuatayo kwenye beti zake:

666 667
Zeinabu:Mungu kesho akipenda Rashidi:Hayo nimeyakariri
Nna safari tanenda Kwenye kitabu vizuri
Shangazi kwenda mtunda Ningojea nisubiri
Salamu meniletea Sote tutajiendea

668 670
Maelezo: Na siku tena nyengine Rashidi: Twende nitakupeleka
Ze'nabu nae anene Upate kwenda kusuka
ZeinabuNataka tukasongane Hayo nimeyaandika
Na shogangu Rukia Kitabuni yamejaa

Kutokana na maelezo ya beti hizo mwanamke amesawiriwa kuwa si mtu wa kuaminika. Na mume awe ni mwenye kufuatilia nyendo zake zote. Ili isije kutokea sababu ya kumwendea kinyume.Mwanamke ni mtu wa kuchungwa saa zote. Hana haki ya kuwa huru. Kwani imeonekana kuwa, kupata uhuru huo ni sababu ya kuvunja uaminifu kwa ndoa yake**.**

**4.2.10 Mwanamke ni kiumbe duni**

Mwandishi ameendelea kusawiri mwanamke katika hali nyengine. Mwanamke ni mtu duni kabisa. Mwanamke kukoseshwa ruhusa kutoka nje, na muda wote kufungiwa ndani. Ushahidi ukurasa 42. Mwanamke ni kiumbe wa kupokea matusi na kipigo katika ndoa. Ushahidi ukurasa wa 54 kama zinavyojieleza:

578 729
Lela: Nafasi yangu ni haba Rashidi:Nyamaza sinighilibu
Nnalo dume jibaba Punda mkosa adabu
Ana wivu kabakaba Zeinabu: Na wewe pia Kidhabu
Milango hunifungia Rashidi: Heshima wanivundia

730
Maelezo: Kwa makelele na mikito
Rashidi katwaa koto
Mkewe kampigato
Hukuno amfokea

Mwanamke ameonekana ni kiumbe duni. Anaekandamizwa na kudhalilishwa kutokana na udhaifu wake. Udhaifu ambao unatokana na utamaduni wa jamii husika. Jamii inayomuona mwanamke ni mtu wa kufungiwa ndani tu. Jamii ambayo inaamini mwanamke anapokosa aadabu ni kipigo.

**4.2.11 Mwanamke ni mtu wa kisasi**

Kwa kuendelea na kumuona mwanamke alivyosawiriwa na mwandishi wa huu *Utenzi wa Vitimbi vya Wanawake.*Mwanamke ni mtu anaeweka kisasi pale anapokosewa. Ushahidi wa haya unaonekana ukurasa wa 50.

681 682
Zeinabu: Basi nitamonyesha Zeinabu: Rashidi anizaini
Tena tamuilimisha Ili nipate kuzini
Asithubutu maisha Japo kuwa sitamani
Wake kuwatunduia Lakini tamzinia

683 684
Zeinabu:Tazini apate koma Zeinabu:Tazini tena bayana
Ajuwe tu wake mama Hata japo taniona
Asitiri zetu tama Atashindwa kupigana
Kashfa kutozitoa Mato atayakodowa

Mwanamke amesawiriwa ni mtu muovu. Akikosewa au akibaini kosa hana njia za usuluhishi ila ni kulipiza kisasi. Na amesawiriwa mwanamke huyo kutojali utu wake. Anapoamua kulipa kisasi hajali kama utu na heshima yake itapotea. Mfumo wa ubabe dume unaonekana kutokujali heshima ya mwanamke. Mfumo huo unamchukulia mwanamke ni mtu asiyejitambuwa, asiyejielewa wala kujithamini utu wake.

**4.2.12 Mwanamke ni mtu wa mipangilio ya uovu**

Mwandishi amemsawiri mwanamke, ni mtu anaethubutu kupanga mipango ya uovu. Mipango ambayo haimrudishi nyuma katika maamuzi yake. Ushahidi wa haya unaonekana ukurasa wa 51,53 na 54 kama zinavyoeleza:

689 690
Zeinabu: Kwa makini pulikiza Zeinabu: Hizino shilingi mia
Haya nitakayokweleza Kibindoni mwako tia
Kisha halafu timiza Masikioyo zibua
Kama nitakavyokwambia Nnaanza kutondoa

691 692
Zeinabu: Hili tikiti tukua Zeinabu: Na hapo penye nafasi
Na kati kulipasua Ya mvungu, weka nsi
Halafu mvungu tia Aenee kwa kiasi
Kiasi kitu kukaa Nde bila kutokea

693 694
Zeinabu:Ukatafute na gamu Zeinabu:Saa kumi ikifika
Tikiti ulilihimu Hapano tena zunguka
Lishikamane timamu Hukuno ukitamka
Mtu bila kuelewa Tikiti nawauzia…

699 714
Zeinabu: Usihofu usijali Maelezo: Alipojiangukia
Jituze ewe rijali Zenabu kajienua
Uko wazi wangu mwili Tikiti kalitukua
Kwa leo niko huria Majini akalitia

715 719
Maelezo: Ndipo maji kalipaka Zeinabu:Shauri nililokata
Hadi likasafishika Tikiti twalolikata
Ile gamu ikatoka Sisi ni kulisakata
Lokuwa mehilimiwa Makini tukajilia

720
Zeinabu: Nakuomba sinipinge
Samaki tumkaange
Usiku tumviringe
Mahamri kutolea

Hivyo mwandishi ameonekana kumsawiri mwanamke kuwa ni mtu mwenye mipangilio ya uovu. Uovu uliokithiri pale anapotaka lake litimie. Mwanamke anaonekana kutokujali utu wake, pale anapoamua kumkomoa mbaya wake. Mwandishi amemsawiri mwanamke ni bazazi wa kauli zake. Analazimisha akitumia ulaghai ndani yake. Mwanamke anapoamuwa lake liwe ni lazima litimie.

Mwandishi Fadhil, amejaribu kiasi cha uwezo wake kumsawiri mwanamke ni mtu wa hali/ tabia alizonazo. Ameonesha kwa jamii kuwa anaonewa na mwanamme. Na mbinu alizozitumia katika kujikomboa na ugandamizwaji huo. kwa njia ambazo hazimstahikii mwanamke huyo. Na katika hali hii ameshindwa kuonesha dhamira aliyoikusudia moja kwa moja kwa wasomaji wake. Na hata kama ipo wasomaji hawatokuwa makini kuliona hilo. Bali umakini wao zaidi kuwepo katika kuzingatia vitimbi alivyonavyo mwanamke na kupokea mafunzo hayo. Hivyo kuonesha kuwa hata huo ukombozi alioukusudia, haukufanikiwa kama alivyokusudia.

Wapo pia waandishi wengine au watunzi ambao wamejaribu kutetea haki za wanawake kwa njia hizo hizo , kama *Utenzi wa kadhi Kassim bin Jaafar* uliotungwa na *Hemed Abdallah bin Said* (2004) na Masimulizi ya *Utenzi wa Ramia bint Daas.* Kwa kudhani kuonesha maovu yao ndio yatasaidia kuwaamsha wanawake hao na kujitetea kwa kutaka ukombozi. Wakati uhalisia wanawake hao huwa tayari wameshadhalilika zaidi.

Hata pale zilipotungwa tenzi zenye kuwaelekeza mema wanawake na namna ya kuishi katika jamii na kuwatunza watu wa familia zao mfano wa *Utenzi wa Mwana Kupona* walizuka wana harakati wa mtazamo kike na kuanza kuzishutumu beti hizo, na kusema zinamdhalilisha mwanamke bila kukaa na kutafakari jamii iliyoandikiwa na wakati ilipoandikwa. Na kuziachilia mbali tenzi

hizi zinazoonekana wazi zimemdhalilisha na kumgandamiza mwanamke.

Kama anavyoelekeza Kitula (2002) kupitia Utenzi huu wa Mwanakupona kuwa ipo haja kubwa ya kuzingatia zaidi matumizi na nafasi ya dini kuliko nadharia za kimagharibi. Ambazo hazionekani kutoa miongozo ya kutosheleza katika uchanganuzi wa jamii za kiafrika.

Zipo tafiti nyingi zilizoandikwa kuona usawiri wa mwanamke kupitia hali mbali mbali kama vile; *Usawiri wa wanawake katika Nguzo mama na Mama Ee*. Iliyotafitiwa na Caleb (2013) na kuonesha namna mwanamke alivyohusishwa tabia zake katika kutetea haki yake.

Momanyi (2002) ameeleza miongoni mwa vigezo vitano vilivyoelezwa na Cheri Register kuhusu masuala ya kike ni kuwa; Fasihi iweze kutoa mifano bora ya wahusika wa kike watakaoweza kuigwa. Hivyo wanapotumiliwa wahusika wa kike watumiwe katika mazingira yanayokubalika zaidi. Anaendelea kwa kueleza kuwa

"Idadi ya wahusika wanawake makahaba pia inasikitisha.
Kwani ukahaba unashurutishwa zaidi kwa wanawake na
kwa hivyo kuwatenga na zile kazi za halali ambazo pia
wangezifanya ili kupata riziki ya kila siku…" (2002: 67)

5.0 Dosari zilizojitokeza

Ni vyema watunzi wanapoamua kutunga kazi zao, kwanza wazifikirie jamii wanazoziandikia, kama anavyoonekana Fadhil alivyoandika kazi yake imejikita zaidi na watu wa pwani kupitia mazingira wanayoishi, majina ya wahusika, lugha aliyotumia ni ya lahaja moja wapo ya maeneo ya mji wa Mombasa Kenya. Na kila atakaesoma kazi hiyo, kuhukumu kuwa mwanamke wa jamii hii, ni mtu muovu. Hivyo kumkashifu mwanamke ni kuikashifu jamii yote kwa ujumla.

Pia waandishi wasiwe ni wenye kuweka mambo kwa ujumla wake, kama mwandishi wa utenzi huu alivyojieleza kuwa makosa ya Sofiya hayawezi kuwa ni makosa ya wanawake wa ulimwengu mzima. Hata hivyo alifikia kuandika baadhi ya beti zake, na kuweka vitimbi hivyo kwa ujumla wake, kuwa wanawake wote ni watu wa vitimbi na vituko. Anaonekana mwandishi ukurasa wa 2, 21, 24 na 42 anaeleza:

| 17 | 292 |
|---|---|
| Salimu:Katika dunia nzima | Salimu: "Leo nimeyaamini" |
| Humpati mke mwema | "Yasemwayo duniani" |
| Hata awe wako mama | "Kwamba wake maluuni" |
| Mwendowe kama wa kaa | "Nami sahihi natia" |

| 329 | 580 |
|---|---|
| Salimu: Mwepushe na marafiki | Lela: Nitakuonya viroja |
| Wanawake wanafiki | Vya wanawake viroja |
| Ingawa hawalindiki | Ujuwe sisi si waja |
| Ovyo si wa kuwatiwa | Ni majini wa dunia |

Mwandishi anaonekana amechupa mipaka, kwa kuamua hata kutoa kashfa za mtu mwenye daraja ya juu katika jamii, anaejulikana ni mama. Ametumia kauli maluuni, kauli ambayo kwa jamii aliyoitumia inaeleweka kuwa ni mtu aliyelaaniwa kama ibilisi wala hana msamaha kwa Mola wake.

Kutokana na maelezo hayo, mwandishi wa makala hii amemuona mwandishi amechukulia mambo kwa ujumla wake. Na la zaidi mwandishi wa utenzi huu ameonekana ana kovu. Kovu ambayo iliathiriwa na mwanamke. Hivyo linapotokea kosa la mwanamke mmoja, huunganishwa ni la wanawake wote. Bila kuzingatia mwanamke huyo ni wa daraja gani; Mama, bibi, mkwe au mke.

Hata hivyo vitimbi walivyonavyo visichukuliwe kuwa ni sehemu ya kutoa machafu yao kwa kuyaanika. Yatolewe kwa njia ya kuelimisha na kuikosoa jamii. Kwa kubainisha pia na maovu ya upande wa pili ambao ni wanaume. Ambapo mara nyingi wao huwa ndio chachu ya maovu hayo yanayofanywa na wanawake.

**6.0 Hitimisho**

Mwandishi Fadhil amejitahidi katika kuonesha ukombozi wa mwanamke. Kwa kuonesha kuwa yumo katika harakati za kusaidia kutetea haki za wanawake. kutokana na Vugu vugu la wanaharakati wa mtazamo kike. Kupitia waandishi mbali mbali ambao walionekana kutetea haki hizo. Haki ambazo zilikuwa zikigandamizwa na kudumazwa kwa kasi na kwa kiwango kikubwa kwa wakati huo. Kutokana na mfumo wa Ubabe dume uliokuwa umetawala katika jamii.

Mwandishi Fadhil ameonekana kushindwa kuwa na suluhisho muwafaka, katika kadhia nzima ya utenzi huu wa Vitimbi vya Wanawake. Kwa kuona njia pekee ni ya kumvua zaidi nguo mwanamke huyo. Na kusababisha kukashifika zaidi badala ya kujikomboa. Ikiwa ni kwa lengo tu, la kutaka kumkomoa mume. Mume ambae alionekana ana wivu kupindukia kutokana na simulizi alizopokea. Pamoja na kupita akivikusanya na kupokea hadithi nyingi. Kutoka vyanzo mbali mbali kuhusiana na wanawake.

Imejitokeza kuwa mbali na kuwa mwanamume amekubali kuwa amepata adabu. Kutokana na kisasi cha mwanamke. Na kuonekana kama mwanamke hajajeruhiwa katika vita vile kwa maelekezo ya mtunzi. Lakini ukweli ni kuwa, mwanamke yule amejeruhiwa, tena vibaya sana kwa kudhalilishwa ujanajike wake. Wakati anaepigwa vita vile, amesitirika.na hatimae kubaini mwenyewe tu kuwa alikuwa akipigwa vita na kutoa tamko katika ubeti wa mwisho uliojitokeza ukurasa wa 59 usemao:

795
Rashidi: Nilikuwa sitambui
Kwamba"Kaiddan nisai"
Waume hatuvijui
Hunna-adhimu" alaa!

Hivyo kwa kumalizia ubeti huu, uliotumia matamko matukufu. Mwandishi wa makala hii ameonelea ni vyema watetezi wanaume. Wanapoamua kutetea haki za wanawake. Iwe kwao ni jambo la busara na hekima kutumia njia muwafaka. Njia ambazo zitakazokuwa hazimkandamizi zaidi mwanamke. Ila kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike ambao watakuwa ni kigezo chema kwa jamii. Ambapo matendo yao ya kishujaa , yatakuwa ni yenye kuigwa na sio ya kashfa na fadhaa.

**MAREJELEO:**


Ameir, A. I (2011) *"Taswira ya Mwanamke katika Riwaya za Bwana Muhammed Said Abdullah".* MAKALA ZA SEMINA YA KUMUENZI MUANDISHI Muhammed Said Abdallah (Bwana MSA). BAKIZA. Zanzibar.

Caleb Ch. Wilson (2013) Utafiti wa *Twasira ya Mwanamke katika Tamthilia ya Nguzo Mama na Mama Ee*. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Fadhil, U. A (1980) *Utenzi wa vitimbi vya Wanawake*. ZANZIBAR PUBLISHERS LIMITED. ZANZIBAR.

Kitula, K (2002) "*Uhakiki wa utafiti kutoka Kenya"*. Utafiti wa Kiswahili. MOI UNIVERSITY PRESS. NAIROBI.

Momanyi, C (2002) "*Swala la uana katika utafiti wa Fasihi ya Kiswahili*". Utafiti wa Kiswahili. MOI UNIVERSITY PRESS. NAIROBI.

Said, H. A (2004) Utenzi wa Kadhi Kassim Bin Jaafar. Chuo cha Uchunguzi cha Lugha Dar es Salaam.

Wafula R. M na Kimani Njogu (2013) "*Nadharia za Uhakiki wa Fasihi"* The Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi.

Wamitila .K.W (2002) *Uhakiki wa Fasihi – Misingi na Vipengele Vyake*-.Phoenix Publishers LTD. Nairobi